JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TANGAZO LA WIKI MAALUM YA NECTA YA HUDUMA KWA WATEJA

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Wiki Maalum ya NECTA ya Huduma kwa Wateja kuanzia tarehe **13 Oktoba, 2025** hadi tarehe **19 Oktoba, 2025** katika Viwanja vya Ofisi za Baraza la Mitihani Mikocheni mkabala na TBC Jijini Dar es Salaam.

Katika Wiki hiyo kutakuwa na utoaji wa huduma za papo kwa papo zikiwemo:

(i) Kupatiwa vyeti mbadala kwa waliopoteza

(ii) Kupatiwa uthibitisho wa matokeo

(iii) Kufanyiwa ulinganifu wa vyeti yaani *equivalence*

(iv) Kufanyiwa marekebisho mbalimbali ya taarifa za usajili kwa wanafunzi

Aidha, katika Wiki hiyo kutakuwa na zoezi maalum la upandaji wa miti katika shule zote za sekondari na msingi pamoja na vyuo vya ualimu nchini ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa Maadhimsho ya Miaka **50** ya Baraza.

Watu wote mnakaribishwa Baraza la Mitihani la Tanzania kwa ajili ya kupata huduma za papo kwa papo kuanzia tarehe **13 Oktoba, 2025** hadi tarehe **19 Oktoba, 2025.**

IMETOLEWA NA:

**KATIBU MTENDAJI**

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze
Kupiga Kura